**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZAMITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE**

**SHULE YA SEKONDARI MSALALA,**
**S. L. P 137,**
**GEITA.**

**Mkuu wa shule +255755277574**
**M/Mkuu wa shule: +255754343112**
**Mtaaluma: +255623361002**
**Barua Pepe:msalalasekondari@gmail.com**

KUMB. Na: MSS/ NDC/ ADM/ F. V/ 2024

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………….
S.L.P………………………….
………………………………..

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MSALALA.**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha **Tano,** Tahasusi ya HGK,HGLna EGM (*kata isiyohusika*) katika shule **ya Sekondari Msalala** mwaka wa masomo **2024/2025.**

## 1.1 MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ipo katika Tarafa ya **Msalala**, Wilaya ya **Nyang'hwale** Mkoa wa **Geita**. Unaweza kuingia Wilaya ya Nyang'hwale ama kwa Kutokea jijini Mwanza au kwa kutokea Geita mjini au kwa kutokea Kahama mjini.Kwa kutokea Mwanza unaweza kufika shuleni kwa kupanda basi la **Asante yesu Express** au **Makingi Express** au **Gajmin express** yanayopatikana katika stand ya mabasi Nyabulogoya (nyegezi) iliyopo jijini Mwanza kuanzaia saa 4 kamili asubuhi mpaka saa 6 kamili mchana. Pia Kwa wanafunzi watakao pititia Geita (Mkoani) watapanda basi la **Shigongo Express**,au **mdabulo express** pia kuna usafiri wa hiace kuanzia saa 2 kamili asubuhi mpaka saa 11 jioni. Kwa wanafunzi watakaotokea Kahama Watapanda Basi la **Bedui Express** au Hiace kuanzaia saa 4 kamili asubuhi mpaka saa 7 kamili mchana. Kutokea maeneo hayo mpaka msalala nauli ni shilingi elfu Saba tu (7,000/=). Kutoka stand ya mabasi kwenda shuleni utapanda bodaboda.

## 1.2 Mihula ya masomo.

Shule itafunguliwa tarehe 13/07/2024 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023

**NB: UNAPOKUJA HAKIKISHA UNAKUJA NA FOMU HII IKIWA NA MAHITAJI YOTE NA IKIWA IMEJAZWA SEHEMU ZOTE.**

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE YA SHULE

- **Mwanafunzi anatakiwa kuja na sare/ mahitaji yafuatayo:-**

i. Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mirefu na yasiyo bana mwili.

ii. Kwa wanafunzi wasio waislamu waje na sketi mbili (2) za rangi ya lightblue mshono wa LINDA BOX makubwa mbele na nyuma na mawili kushoto na kulia mawili na tai mbili zenye rangi ya sketi (light blue), urefu wa sketi uwe unaofika katika vifundo(enka) vya miguu

iii. Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na;

- **Blauzi (Nusu Kanzu 2) rangi nyeupe.**
  Iwe na mikono mirefu isiyofunika vitanga (Viganja) vya mikono
  Iwe pana isibane
  Iwe ndefu inayoshuka chini ya makalio (isiwe kama gauni)
  Isiwe nyepesi
- **Hijab (Ushungi, 2) uwe wa rangi nyeupe.**
  Kiwe kipana
  Kiwe kirefu hadi usawa wa tumbo.
- **Sketi mbili (2) rangi ya lightblue**
  Iwe ni yenye urefu unaofika katika vifundo vya miguu
  Iwe pana na isiwe nyepesi
- Hijab ya kushindia iwe nyeusi au darkblue

iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi. **Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo wa aina yoyote.**

v. Jozi mbili (2) za soksi nyeupe ndefu zisizo na mistari yoyote.

vi. Nguo za kushindia (shamba dress) gauni mbili za rangi ya kijivu, mshono wa solo, kitambaa aina ya Kunguru. T-shirt za rangi ya ugoro zenye kola.

vii. Sweta rangi ya ugoro.

viii. Shuka mbili (2) rangi ya blue bahari (light blue), Kwa mwenye matatizo ya kiafya anaruhusiwa kuja na blanketi (Siyo lazima)

ix. Godoro la ukubwa wa futi 2.5x6.

x. Tracksuit rangi ya blue bahari (light blue) Jozi moja atavaa wakati wa maandalio ya usiku (Night preparation) na siku za michezo.

xi. Tranka ( sanduku la chuma) na kufuli kwa ajili ya usalama wa vitu vyake.

xii. Chandarua rangi ya light blue

xiii. **Mavazi ya michezo:** Raba, T-shirt (Light blue), vifaa vingine kwa michezo ya kipekee.

xiv. File kwa ajili ya kutunzia taafa zake.

xv. Mwanafunzi aje na nakala za vyeti vifuatavyo
- Cheti cha kuzaliwa (birth certificate)
- Cheti cha kumaliza elimu ya sekondari (Leaving certificate)
- Cheti cha awali cha taaluma (results slip)
- Namba ya NIDA ya mzazi/wazazi.

**UVAAJI WA SARE YA SHULE**

**Sare ya shule ivaliwe wakati wote wa masomo,baraza,mihadhara,na wakati mwanafunzi anapokwenda nje ya mipaka ya shule.T-shirt ya shule ivaliwe ndani tu wakati usio wa masomo na sweta ivaliwe wakati wa baridi tu.majaketi,makoti,kofia,na mapambo mengine haviruhusiwi kuvaliwa kabisa pamoja na sare ya shule.hivyo atakayeonekana na mavazi mengine tofauti na yasiyo ainishwa hapo juu atachukuliwa hatua za kinidhamu.hakuna nguo zitakazoruhusiwa tofauti na sare za shule.**

**2.2 Mahitaji mengine ya mwanafunzi**

i. Vyombo vya chakula (sahani, kijiko, kikombe na bakuli )

ii. Ndoo mbili za lita 10 kwa ajili ya usafi na maji ya kunywa.

iii. Picha 4 passport size (kwa ajili ya kurahisisha utengenezaji wa kitambulisho zitapigwa shuleni akiwa kwenye sare za shule)

iv. Madaftari 11 (counter Book) quire 3 au 4, kalamu za risasi, wino na mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical set). (Kwa wanafunzi wa EGM)

v. Madaftari 11 (counter Book) quire 3 au 4, kalamu za risasi na za wino (Kwa wanafunzi wa (HGL, HGK)

vi. Calculator kwa wanaosoma masomo ya uchumi na Hesabu (scientific calculator) (Iwe ni FX = 991)

vii. Mwanafunzi wa EGM aje na jembe na mpini 01, HGL aje na fyekeo 01, na mwanafunzi wa HGK aje na squeezer 01

viii. Mwanafunzi aje na limu moja aina ya A4 ( kwa kila mhula) kwa mwaka ream mbili

ix. Mwanafunzi aje na mfagio wa chelewa wenye mti wa kushikia

x. Nwanafunzi aje na mfagio wa ndani (soft bloom)

**2.3** Vifaa mhimu vinavyopatikana katika mazingira ya shuleni

i. Sketi rangi ya bluu bahari

ii. Sweta rangi ya ugoro zenye nembo ya shule

iii. Nguo za kushindia (shamba dress)

iv. Jembe na mpini

v. Mfagio wa nje (chelewa ya mti) na mfagio wa ndani (soft bloom)

vi. T-shirt rangi ya ugoro
vii. Chandarua (mosquito net)
viii. Fyekeo
ix. Reki

NB: Mwanafunzi anashauriwa kupata sare shuleni au kufanya mawasiliano ili kuepuka usumbufu unaowezakujitokeza kutokana na mkanganyiko wa rangi ya sare.

**3.0 Michango inayotakiwa kulipwa na kila mwanafunzi kupitia benki**

| NA | AINA YA MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| **1** | **UENDESHAJI** | **65,000/=** |
| **2** | **TAHADHARI** | **5000/=** |
| **3** | **NEMBO** | **5000/=** |
| **4** | **KITAMBULISHO** | **5000/=** |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**BIMA YA AFYA**: Hakikisha binti yako anakuja na bima ya afya shuleni yaweza kuwa NHIF au CHF kwa ajili ya matibabu kama hana bima ya afya atalazimika kuja na **tsh 5,000**/= mkononi itakayolipwa kwa ajili ya bima ya CHF. **BIMA NI LAZIMA**

**4.0** Michango hii ilipwe kwenye akaunti ya shule, **Msalala Secondary School, A/C No. 31001100575** katika banki ya **NMB** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip). **FEDHA INAYOPOKELEWA MKONONI NI YA BIMA TU**

**5.0 SEHEMU AMBAZO WANAFUNZI HAWARUHUSIWI KUFIKA BILA KIBALI**

- Chumba cha walimu (Staff room)
- Maabara
- Ofisi ya shule
- Jikoni
- Nyumba za walimu na wafanyakazi

**6.0 SEHEMU ZILIZOPIGWA MARUFUKU WANAFUNZI KUTEMBELEA**.

- Vilabu vya pombe
- Majumba ya starehe (Clubs)
- Nyumba za kulala wageni.

**7.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**.

Makosa yaliyoorodheshwa hapa chini yanasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule bila onyo.

- Wizi.
- Kutohudhuria shule masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
- Kugoma na kuhamasisha mgomo.
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
- Kupigana/kupiga mwanafunzi, mwalimu au/na mtu yeyote yule.
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- Uvutaji wa sigara.
- Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuolewa.
- Kupata ujauzito au kutoa mimba.
- Kushiriki kutoa mimba
- Kushiriki matendo ya uhalifu, makosa ya jinai na uvunjaji wa sheria za nchi.
- Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- Kumiliki au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- Kudharau Bendera na wimbo wa Taifa
- Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- Uhalibifu wa mali ya umma kwa makusudi
- Kukataa adhabu
- Kukutwa nje ya mipaka ya shule bila ruhusa au kibali.

**ANGALIZO**:Mwanafunzi atakayebainika/kukamatwa na simu atatozwa faini ya shilingi laki mbili tu (200,000/= Hivyo mzazi hakikisha mwanao hamiliki simu kwa namna yoyote ile ili kuepuka kuisababishia familia hasara isiyo ya lazima.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MSALALA**

**MAURICE. O, MAIRA**

**MKUU WA SHULE**

**FORM NO. 1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENTS' OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MSALALA SECONDARY SCHOOL,**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

A. To be completed by a medical Officer in respect of all Form V entrants.
   - Pupil's name…………………………………………………………………………
   - Age/Years……………………………………Sex…………………………………
   - Blood found (red and whiteWhite)………………………………………………………….
   - Stool examination:…………………………………………………
   - Urinalysis:………………………………………………………………
   - VenerealDiseasestest:…………………………………………………………………
   - T.B.test:………………………………………………………………………………
   - EyeTest:………………………………………………………………………………
   - Ears:…………………………………………………………………………………
   - Chest:…………………………………………………………………………………
   - Spleen:………………………………………………………………………………
   - Abdomen:……………………………………………………………………………
   - UrineforPregnant:……………………………………………………………………

B. ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

   ………………………………………………………………………………………..
   …………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………
   …………………………………………..

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.
Signature:…………………………………………………………..
Designation:………………………………………………………..
Station:…………………………………..Date:……………………
Official Stamp:

**FORM NO.2**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE**
**MSALALA SECONDARY SCHOOL**
**P.O. Box 137, Tel: +255755277574, GEITA**

**JINA ………………………………………………KIDATO:………… MCHEPUO:……...**

a) Jina kamili la Baba:……………………………………
Anuani :……………………………………………..
Simu:…………………………………………………..
E-mail:…………………………………………………
Namba ya NIDA…………………………………………
Uhusiano:…………………………………………………
Sahihi:…………………………………………………
Tarehe…………………………………………………

PICHA YA HIVI KARIBUNI

b) Jina kamili la Mama:…………………………………..
Anuani :……………………………………………..
Simu:…………………………………………………..
E-mail:…………………………………………………
Namba ya NIDA…………………………………………
Uhusiano:………………………………………………….
Sahihi:…………………………………………………
Tarehe…………………………………………………

PICHA YA HIVI KARIBUNI

**WALEZI**

a) Jina kamili la mlezi:……………………………………
Anuani :……………………………………………..
Simu:…………………………………………………...
E-mail:…………………………………………………
uhusiano:…………..……………………………….
Sahihi:………………………………..………………
Tarehe:…………………………………………………

PICHA YA HIVI KARIBUNI

b) Jina kamili la mlezi:……………………………………
Anuani :……………………………………………..
Simu:…………………………………………….....
E-mail:…………………………………………………
uhusiano:………………….……………………………….
Sahihi:………………………………………………..
Tarehe:…………………………………………….....

PICHA YA HIVI KARIBUNI

**NB:*Wazazi na walezi ni muhimu mjaze fomu hii kwa usahihi na ukamilifu. Ninyi ndio mtakaotambuliwa rasmi na Shule***

**FORM NO.3**

## SHULE YA SEKONDARI MSALALA

## MKATABA/ AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi…………………………………………. (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Nahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Saini ya mwanafunzi………………………………………

Tarehe………………………………………………………

Shahidi

Jina kamili…………………………………………………

Saini……………………………………………………….

Tarehe………………………………………………………

**SHULE YA SEKONDARI MSALALA**

**FORM NO. 4**

**A: AHADI YA MZAZI:**

Mimi………………………………………………… (jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa……………………………………..Kidato cha…………………. Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliananayote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

Saini ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………….

Anuani kamili……………………………………………………………………

Simu:…………………………………………

Tarehe:……………………………………….

**FORM NO 5**

## SHERIA, KANUNI NA MWENENDO BORA WA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyo lekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na teknolojia , yenye zamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAIS –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshajiwa elimu.

**1.0 Unapojiunga na Shule.**

Kila mwanafunzi anayejiunga na shule hii anapaswa kutambua kuwa yupo hapa kwa ajili ya KUSOMA kwa faida yake (familia yake) na Taifa lake kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, chochote kilichopo nje ya jukumu hili hakina nafasi katika shule hii, kiwe kwa maneno au kwa vitendo.

**2.0 Kuwahi na mahudhurio ya kila siku.**

a) Kuwahi shuleni ni wajibu wa kila mwanafunzi, hivyo kila mwanafunzi anapaswa kuripoti shuleni tarehe ya kufungua shule bila kukosa na kuendelea kuwepo shuleni kila siku.

b) Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na nje ya darasa. Vipindi vya kazi za mikono pamoja na michezo ni sehemu ya masomo. Ni wajibu pia kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazopewa na Shule.

c) Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria mikusanyiko halali yote ya shule kama vile, mstarini(parade), usafi, Baraza la shule, Ibada, midahalo (Debates), n.k.

d) Ni lazima kutimiza kwa makini mahudhurio ya maandalio ya jioni (Evening Preparation).

e) Ni lazima mwanafunzi ahifadhi vitu vyake na kulala bwenini. **’Bed Check’** na ’**Inspection’**-**ukaguzi utafanyika mara kwa mara (angalau mara moja kwa mwezi) na wakati wowote bila taarifa**.

f) Kila mwanafunzi anawajibika kuwahi kula chakula kwa wakati uliopangwa. Ni marufuku kuwahi kuchukua chakula kabla ya wengine wote bila kibali maalum. Tatizo lolote liripotiwe kwa mwalimu wa zamu / wa chakula kwanza.

**3.0 Heshima, adabu na Utii.**

a) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema popote alipo ndani na nje ya mipaka ya shule.

b) Kila mwanafunzi anatakiwa kutii kengele, kutii na kuwaheshimu walimu, wafanyakazi wote, Viranja wa shule na Jumuiya nzima ya msalala sekondari.

c) Mwanafunzi anatakiwa kusimama /kumpokea na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita au aingiapo shuleni, darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
d) Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, fedha za Taifa, Wimbo wa Taifa, Wimbo wa Shule, Nembo ya Taifa na Picha za viongozi wa Serikali.
e) Wanafunzi wakati wote wawe na heshima kati yao wenyewe na kwa walimu na wafanyakazi wasio waalimu pia. Hairuhusiwi kwa wanafunzi kugombana au kufanya malumbano ya kidini, kikabila au mfano wa hayo.
f) Kiranja yeyote wa shule anatakiwa kula kiapo cha utii na kuwa mfano katika kutekeleza kanuni na taratibu za shule. Kukiuka taratibu za shule kunaweza kumpotezea sifa ya kuwa kiongozi na adhabu nyingine kuchukuliwa dhidi yake ikiwa pamoja na kusimamishwa / kufukuzwa shule. Mkuu wa shule ana mamlaka ya kuteua kiongozi mwingine wakati wowote pale itakapobidi.

**4.0 Sehemu Muhimu za Kujifunzia kama Madarasa, Maabara na Maktaba.**

Madarasa, Maabara na Maktaba ni sehemu za masomo, hivyo ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele, kuzomea, kupiga gumzo au kuzurura ndani ya sehemu hizo. Hairuhusiwi kutumia viti na madawati kusomea nje ya madarasa au ukumbi wa mkutano bila ya kibali. Ikithibitika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.

a) Ni marufuku kuingia kwenye Maabara bila ya kibali cha mwalimu husika.
b) Ni lazima kila mwanafunzi atumie Maktaba kufuatana na sheria za maktaba.
c) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuandika ubaoni bila ya kibali cha mwalimu. Ni vyema mbao zote zifutwe baada ya kila kipindi au muda wa darasa unapokwisha.

**5.0. VITU VISIVYO RUHUSIWA**

Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki vitu vifuatavyo akiwa shuleni;-

a) Simu
b) Pasi ya umeme
c) Heater
d) Redio

**NB: Pasi ya mkaa inaruhusiwa**